wanyama mara inapolazimu ili kupunguza nyasi na kuipa mikunde nafasi nzuri ya kustawi.

## Uzuiaji wa magugu na vichaka

Hakikisha kwamba umeondoa magugu na vichaka kwenye shamba lako ili malisho yaweze kustawi vema.

## Uwekaji wa mbolea

Unapotumia malisho kwa kuchungia au kukata, rutuba ya udongo hupungua. Hivyo ni muhimu kuwekea mbolea ili kurudisha rutuba ya udongo.

## Utumiaji wa malisho

Malisho yanaweza kutumiwa kwa njia aidha ya kuchungia moja kwa moja, kuyakata na kuyafunga mithiri ya mkate (hay bales) na au kuhifadhi humo humo shambani pasipokuchungia kwa muda maalum.

## Kuchungia

Chunga wanyama wako kwa kufuata utaratibu ambao utahakikisha kwamba aina zote za malisho ulizopanda haziharibiwi kwa kuweka idadi ya wanyama kulingana na wingi wa malisho yaliyopo katika eneo.

## Kuhifadhi malisho

Ni jambo la busara kuhifadhi malisho ya ziada kwa matumizi ya baadaye hasa wakati wa uhaba (Kiangazi). Njia zifuatazo hutumika katika kuhifadhi malisho: “Hay” na au “Silage”.

## “Hay”

‘Hay” ni malisho yanayokatwa hasa mwanzoni mwa Kiangazi katika hali ya ubichi kwa kutumia vifaa kama vile panga, mundu, visu, au mashine na kunyaushwa kwenye mwanga wa jua bila



Figure 4: Shamba la malisho (nyasi) lililovunwa na kufungwa hay

kupoteza ukijani wake. Hatimaye huhifadhiwa kwa matumizi ya baadaye wakati wa uhaba wa malisho kufungwa mithiri ya mkate kwa kutumia aidha mashine maalum au njia nyinginezo.

## “Silage”

“Silage” ni malisho yanayokatwa mwanzoni mwa kutoa maua na baadaye kukatwa katwa katika vipande vidogo vidogo. Hatimaye hujazwa kwenye shimo liitwalo “Silo”, kushindiliwa ili shimo liweze kuwa na uwezo wa kuchukua malisho mengi na pia kuondoa hewa, na kufunikwa kwa kutumia majani makavu na udongo. Chakula hiki huwa tayari kwa kulishia mifugo baada ya miezi 6 na kuendelea.

*This information is partly drawn from experiences from the project on “Crop-livestock integration for sustainable management of natural resources and building livelihoods resilience in Eastern and Central Africa” of the Livestock and Fisheries Programme of ASARECA*

ASARECA
Transforming Agriculture for Improved Livelihoods

# Ustawishaji, utunzaji na utumiaji wa malisho bora ya mifugo



## Utangulizi

Zaidi ya asilimia 60 ya eneo la ardhi hapa nchini ni mbuga za malisho ya asili ambayo hutegemewa kwa chakula na mamilioni ya mifugo na wanyama pori. Walakini malisho haya hukomaa na kukauka mapema zaidi na hivyo kusababisha lishe yake kuwa duni na ustawi hafifu kwa wanyama wanaoyatumia hususani nyakati za kiangazi kikali na cha muda mrefu ambapo wanyama huhangaika sana kupata chakula (malisho) hicho. Kutokana na upungufu wa ubora wa malisho haya, upo umuhimu wa kuotesha aina bora za malisho.



Mifugo wakihangaika kutafuta chakula (malisho) wakati wa kiangazi kikali maeneo ya Mabuki

## Uoteshaji

Hatua zifuatazo huzingatiwa wakati wa uoteshaji wa malisho:

Utayarishaji wa shamba, Kurutubisha ardhi na upandaji.

## Utayarishaji wa Shamba

Endapo shamba lako lina miti au vichaka yabidi kwanza lisafishwe ili kurahisisha ulimaji. Shamba laweza kusafishwa kwa kutumia moto, kufyeka na kung'oa au njia zote tatu kwa pamoja. Baada ya kusafisha, kazi inayofuatia ni kulima tayari kwa upandaji. Ulimaji waweza kufanyika kwa kutumia jembe la mkono au plau ya ng'ombe au trekta. Hakikisha umepiga harrow ili kulainisha udongo ili kurahisisha uotaji wa mbegu za malisho ambazo nyingi huwa na umbo dogo.

## Kurutubisha ardhi

Ni muhimu kurutubisha udongo ili kurekebisha upungufu wa madini mbalimbali yanayohitajika na mimea. Katika kufanya hivyo waweza kutumia Samadi, mboji au mbolea za chumvi chumvi.

## Upandaji

katika upandaji wa mbegu za malisho mambo yafuatayo ni muhimu: ubora wa mbegu, wakati wa kupanda, na njia za kupanda.

## Ubora wa mbegu

Hakikisha kwamba umepata mbegu za kupanda kwenye shamba lako kutoka mahali panapoaminika kama vile Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Mabuki, vituo vya Utafiti wa Malisho ya Mifugo kama Kongwa (Dodoma), vituo/mashamba ya kuzalisha mbegu za malisho ya mifugo kama vile Vikuge (Dar-Es-salaam), Langwila (Iringa) n.k. nchini Tanzania; Taasisi za Utafiti wa Kilimo na Mifugo Namlonge and Serere Mbegu na pia kutoka kwa Wakulima nchini Uganda; na nchini Kenya mbegu hizi hupatikana kutoka katika Taasisi za Utafiti wa Kilimo na Mifugo kama KARI pamoja na Makampuni yanayozalisha mbegu ya malisho ya mifugo. lazima ziwe ni zile zinazoweza kuota vizuri, zisizo na mbegu za magugu na pia zisiwe na magonjwa au wadudu.

## Wakati wa Kupanda

Panda mbegu zako mara tu mvua zinapoanza na wakati ambapo kuna uwezekano wa mvua kuendelea kunyesha angalau kwa miezi 3 mfululizo. Hii itakuhakikishia uotaji na ustawi wa mbegu zilizopandwa.

## Njia za Kupanda

Katika upandaji njia zifuatazo zaweza kutumika; kusia (broadcasting) na kupanda kwa mstari uliochorwa kwa kuchimba/kuparaza kidogo ardhini (drilling).

## Kusambaza, kutupia au kusia mbegu katika shamba (broadcasting)

Wakati wa kupanda kwa njia hii, changanya mbegu na mchanga au unga wa mbao (Saw dust). Hii itarahisisha uenezaji wa mbegu vizuri. Pia itazuia mlundikano wa mbegu nyingi sehemu moja na kupunguza matumizi ya mbegu nyingi isivyostahili. Baadaye unaweza kuwaruhusu mifugo wadogo kama vile mbuzi au ndama kupitia pale palipopandwa mbegu hizi humo shambani kwako, na au ukiweza, pitisha/buruta tawi la mti lenye miiba. Hii ina madhumuni ya kufunika mbegu ili zisiweze kupeperushwa na upepo na au kufukiwa zaidi na hivyo kuzifanya kushindwa kuota/kutokeza na kuendelea kustawi juu ya ardhi.

## Kupanda kwa kumimina mbegu kweye mstari/kijimtaro (drilling)



Shamba la malisho jamii ya mikunde (Legume – Lablab purpureus) lililooteshwa kwenye kimfereji

Chora mstari kwa kutumia Kijiti, kisha mimina mbegu kwenye mstari huo halafu funika. Ni muhimu kuchanganya mbegu na mchanga au unga wa mbao (Saw dust) ili kuzuia mlundikano wa mbegu nyingi sehemu moja na pia kupunguza matumizi ya mbegu isivyostahili. Pia baada ya hapo unaweza kufanya kama hapo juu.

## Kupanda kwa kutumia vikonyo vya mmea ambao tayari umeota (Transplanting)

Chimbua kishina cha mmea ambao tayari umeota, kisha kigawe hicho kishina katika vishina vidogo vidogo ambavyo hivyo ndivyo hupandikizwa kwenye udongo na mvua zikinyesha vizuri, kila kishina kilichopandwa huchipuka na kuota na kuwa mmea kamili

## Utunzaji

Hakikisha kwamba shamba lako lililooteshwa mara ya kwanza linaachwa angalau kwa msimu mmoja bila kuchungiwa ili mbegu zilizokomaa zidondoke kwa kuota msimu ujao. Endapo kuna mchanganyiko wa nyasi na mikunde inashauriwa kuchungia kundi la



Malisho jamii ya nyasi (Grass spp – Chloris gayana) yaliyooteshwa kwa kutumia vikonyo/vishina